



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA



Unapojibu, tafadhali taja:
Kumb. Na. CDA.156/234/21/195

11 Oktoba, 2022

Katibu Mkuu,
Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara,
Mji wa Serikali, Eneo la Mtumba,
S.L.P 2996,
40480 DODOMA

**YAH: MALALAMIKO YA MWEKEZAJI KAMPUNI YA AL HUSHOOM
INVESTMENT (T) LTD**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

- Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimepokea barua yako yenye Kumb. Na.CGA.68/157/01 ya tarehe 11 Oktoba, 2022 kuhusu malalamiko ya mwekezaji wa kampuni ya Al Hushoom Investment (T) Ltd.
- Kituo kinapenda kukujulisha kuwa mwekezaji husika suala lake linafanyiwa kazi na amejulishwa kwa barua yenye Kumb, Na. Na.TICC/PP.10/07169-1/09 ya tarehe 07 Oktoba, 2022 ambayo pia umenakiliwa kuhusu maombi yake ikimtaka kuwasilisha nyaraka muhimu za sababu za mradi kutokutekelezwa kwa wakati kwa kuwa muda wa utekelezaji wa mradi kutumia vivutio vya kikodi ulishaisha. Ifahamike kuwa wawekezaji wanaoomba kuongezewa muda wa ziada kutumia vivutio wanaombwa nyaraka muhimu kutokana na sababu wanazokuwa wametoa na ndicho kilichotokea kwa mwekezaji husika.
- Aidha, kwa kuwa barua yako imeelekeza TIC kuhuisha Cheti bila kurejea barua ya TIC kwenda kwa mwekezaji na nakala katika ofisi yako. Kituo kimeona ni vema kuwepo na ufahamu wa pamoja wa maombi husika kabla ya kutoa cheti bila nyaraka muhimu. Nakala iliyowasilishwa kwa mwekezaji imeambathishwa kwa rejea
- Tutashukuru kwa muongozo wako.

P. Maganga
Kny: MKURUGENZI MTENDAJI



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.TICC/PP.10/07169-1/09

07 Oktoba, 2022

Mkurugenzi Mtendaji,
Al Hushoom Investment (T) Limited,
S. L. P. 20831,
DAR ES SALAAM

**YAH: MAOMBI YA KUONGEZA MUDA WA UTEKELEZAJI MRADI KATIKA CHETI CHA
VIVUTIO VYA UWEKEZAJI**

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu,

2. Rejea maombi yako kwa njia ya mfumo kuomba TIC ikupatie cheti kipya cha Vivutio vya Uwekezaji kwa mradi wa sekta ya usafirishaji ambapo TIC ilikujulisha kwa njia ya mfumo wa usajili kuwa haiwezi kusajili mradi wako kama mradi mpya kwa kuwa tayari mradi wako upo na umesajiliwa TIC.
3. Aidha, mnamo tarehe 22.09.2022 Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kilipokea barua yako ya kuomba kuongezewa muda wa utekelezaji wa mradi huo huo. Kituo kwa kuwa kilipokea maombi yako kwa njia ya kawaida ilikujulisha kwa barua ya tarehe 27.09.2022 yenye Kumb. Na.TICC/PP.10/07169-1/08 kuwa maombi yote kuhusu Cheti cha Vivutio yanashughulikiwa kwa njia ya kieletroniki hivyo ulijulishwa kupitisha maombi husika kwa mtandao.
4. Hivyo, TIC ilipokea maombi yako kwa njia ya mfumo wa kieletroniki yenye barua yenye Kumb. Na AHITL/TIC/001/2022 na viambatanishi kuomba kuongezewa muda wa utekelezaji wa mradi kwa Cheti cha Vivutio vya Uwekezaji (Certificate of Incentives) Na. 070169-1 cha mwaka 2014 ili kuweza kuendelea na utekelezaji wa mradi wako kwa kutumia vivutio ambavyo ulishapatiwa zamani.
3. Tunapenda kukufahamisha kuwa kwa hali ya kawaida cheti husika kinatolewa kwa lengo la kupatiwa vivutio vya kikodi kwa muda wa juu wa miaka mitano (5) toka kusajiliwa. Hata hivyo iwapo mwekezaji atakuwa na sababu maalum zilizosababisha kuchelewa kutekelezwa kwa mradi, TIC inaweza kuongeza muda wa utekelezaji kwa zaidi ya miaka mitano (5).
4. Kama unavyofahamu, mara baada ya kuwasilisha ombi lako, TIC imefanya jitihada mbalimbali kulishughulikia ikiwepo kutembelea eneo la mradi ili kujiridhisha na hali ya utekelezaji mradi (Project Verification Visit - PVV) na kupitia PVV hiyo, tulikuomba nyaraka mbalimbali ili kupata uthibitisho unaoonyesha sababu maalum zilizosababisha kuchelewa utekelezaji mradi ambazo bado hazijawasilishwa.

5. Kwa mantiki hiyo, Kituo katika kuhakikisha kinasaidia wawekezaji kinaomba kupatiwa nyaraka za ziada kama uthibitisho wa sababu za kushindwa kutekeleza mradi kwa wakati kama uwezo wa kifedha kwa sasa, mkataba wa mkopo, mikataba ya kazi za zabuni za huduma ya usafirishaji, mikataba iliyositishwa awali au nyaraka zozote muhimu zitakazoweza kukamilisha maamuzi ya ombi lako.

6. Nakushukuru kwa ushirikiano wako,



A.E. Lyimo

KNY: MKURUGENZI MTENDAJI

Katibu Mkuu,
Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara,
Mji wa Serikali, Eneo la Mtumba,
S.L.P 2996,
40480 DODOMA